BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA USTAWI WA JAMII KUHUSIANA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** Kwanza kabisa naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Allah Subuhanahu Wataala, Muumba Mbingu na Ardhi pamoja na viumbe vyote, kwa kutujaalia uhai na afya njema na kuweza kukutana katika Baraza hili la Kumi, kwenye Mkutano huu wa Kumi na Moja kwa lengo la kuwatumikia wananchi wetu wa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** Vile vile, nakushukuru wewe Mheshimiwa Spika pamoja na wasaidizi wako wote kwa kuliongoza Baraza hili tukufu, kwa umahiri na weledi wa hali ya juu. Nikiamini kwamba uadilifu wenu huo wa hali ya juu ndio chachu ya kuimarika kwa Demokrasia katika muhimili huu muhimu wa dola katika nchi yetu hii.

**Mheshimiwa Spika,**
Aidha, nachukua fursa hii adhimu kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi kwa kazi nzuri na kubwa ya kutuletea maendeleo nchini. Vile vile, tunawapongeza wasaidizi wake Makamu wa Kwanza wa Rais Mhe. Othman Masoud Othman na Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Hemed Suleiman Abdulla kwa kumsaidia vyema Mhe. Rais wetu katika kutekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** Pia, sina budi kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na watendaji wao wote wakiongozwa na Katibu Mkuu pamoja na watendaji wa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa mashirikiano waliyotupatia wakati wa kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya Wizara hii.
**Mheshimiwa Spika,** Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yangu kwa kuniamini na kunipa mashirikiano mazuri ambayo yameniwezesha kufanikisha kazi zangu kwa wepesi. Kwa hakika ni wajumbe mahiri wenye uweledi, wameweza kuijadili ipasavyo na kuhoji

mambo mbali mbali kwa lengo la kuhakikisha kwamba fedha wanazoidhinisha kwa Wizara hii zinatumiwa kwa matumizi yaliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa heshima na taadhima, napenda kuwatambua Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yetu kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Mohamed Ahmada Salum - Mwenyekiti
2. Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Abdalla Abasi Wadi - Mjumbe
4. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Mjumbe
5. Mhe. Haji Omar Kheri - Mjumbe
6. Mhe. Zawadi Amur Nassor - Mjumbe
7. Ndg. Fatma Omar Ali - Katibu
8. Ndg. Mussa Issa Mussa - Katibu
9. Ndg. Azmina Hamad Khamis - Msaidizi

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya kumaliza utangulizi, sasa naomba nichukue nafasi hii adhimu kutekeleza jukumu lililonileta hapa mbele ya Baraza lako tukufu, kwa ajili ya kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka wa fedha 2023/2024 katika fungu lake (*vote*) ambalo ni K01 imepanga kutekeleza Programu Kuu Sita (6) zenye Programu Ndogo Tisa (9) ambapo kwa ujumla fedha zilizoombwa ni **shilingi 457,299,603,000/= (Bilioni Mia Nne Hamsini na Saba, Milioni Mia Mbili Tisiini na Tisa, Laki Sita na Elfu Tatu).** Wakati mwaka jana ilipangiwa jumla ya **shilingi 309,815,073,000/= (Bilioni Mia Tatu na Tisa, Milioni Mia Nane na Kumi na Tano na Elfu Sabiini na Tatu).**

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa upande wa mapato Kamati inaipongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kuweza kukusanya kiwango walichokadiriwa kwa mwaka wa bajeti 2022/2023 cha **Tsh. 396,396,000/= (Milioni Mia Tatu na Tisiini na Sita, Laki Tatu na Tisini na Sita Elfu),** ambapo hadi kifikia Machi 2023 Wizara tayari imekusanya jumla ya **Tsh. Milioni 267,496,320/= (Milioni Mia Mbili na Sitini na Saba, Laki Nne na Tisiini na Sita, Mia Tatu na Ishirini)** sawa na asilimia 72.4.

**Mheshimiwa Spika,**
Licha ya pongezi hizo, Kamati inaishauri Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango wakati wanapopanga vyanzo vya mapato kwa Wizara kuwashirikisha kikamilifu watendaji wa wizara husika ili kuondoa malalamiko ya kupangwa kwa viwango vikubwa vya mapato kinyume na uhalisia wa makusanyo wanayokusanya.

## PROGRAMU KUU YA MAANDALIZI NA MSINGI

**Mheshimiwa Spika,** kupitia utekelezaji wa Programu Kuu hii ya **PK0101**, Kamati inachukua fursa hii kuipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Mhe. Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi kwa kuona umuhimu wa kuelekeza fedha za Ahueni ya UVIKO 19 kwa ajili ya Miradi ya Ujenzi wa Majengo 21 ya Skuli za Msingi na Sekondari kwa Unguja na Pemba.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na pongezi hizo, Kamati inaiomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuzisimamia na kuziendeleza Skuli hizo ili ziweze kufikia azma na malengo yaliyokusudiwa ya kupunguza msongamano wa idadi kubwa ya wanafunzi ndani ya madarasa ili wanafunzi wapate kusoma katika mazingira salama na rafiki kwao na kujipatia elimu iliyo bora.

## PROGRAMU KUU YA ELIMU MBADALA NA MAFUNZO YA AMALI

**Mheshimiwa Spika,** Programu Kuu hii inatekelezwa kupitia Programu Ndogo mbili (2) ambazo ni **SK010401** Programu Ndogo ya Elimu Mbadala na Watu Wazima na **SK010402** Programu Ndogo ya Elimu ya Mafunzo ya Amali ambapo huduma zinazotolewa ni kutoa mafunzo ya kujua kusoma, kuandika na kuhesabu kupitia Mfumo Mbadala wa Elimu pamoja na kutoa Mafunzo ya Amali kwa vijana wetu ili baadae waweze kujiajiri na kuajirika kama ilivyoelezwa katika Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.

**Mheshimiwa Spika,** Katika Programu hii Kamati itajielekeza zaidi katika **Programu Ndogo ya SK010402** ambayo inahusiana na Elimu ya Mafunzo ya Amali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati hadi inawasilisha Hotuba hii ya Maoni kuhusu Bajeti ya Wizara hii haijaridhishwa na usimamizi na uendeshaji wa Vyuo vya Amali vilivyopo Unguja na Pemba. Licha ya kutengwa kwa fedha nyingi zinazokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa ajili ya "*Skill Development Levy*" lakini mfumo wa upatikanaji wa fedha hizo umekuwa haufahamiki hali inayopelekea Vyuo hivi kushindwa kujiendesha kwa ufanisi zaidi kama ilivyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Vile vile**,** kutokana na ukosefu wa fedha hizo zinazokusanywa kwa ajili ya kuviendeleza Vyuo hivyo, Kamati imebaini kwamba bado Vyuo hivyo vinakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo ukosefu wa vifaa vya kufanyia mafunzo ya vitendo pamoja na uhaba wa walimu waliobobea katika fani zinazotolewa ndani ya Vyuo hivyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali fedha zote zinazokusanywa kwa ajili ya "*Skill Development Levy*" zielekezwe katika kuimarisha miundombinu ya Elimu ya Mafunzo ya Amali kwa asilimia 100.

## PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA ELIMU

**Mheshimiwa Spika,** Katika **Programu Kuu** hii ya **PK0106**, Kamati inajikita katika kuzungumzia **Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji** ambayo ni **SK010601** pamoja na **Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara SK010602**.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapendekeza kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kupitia Idara ya Utawala na Uendeshaji kuandaa utaratibu maalum kwa walimu wote wanao ajiriwa kuanzia sasa kuwepo na sharti la kuwa na leseni halali za Ualimu kabla ya kuanza kazi ili kupunguza changamoto za walimu wasiokuwa na sifa za kusomesha. Kufanya hivyo kunapelekea kuongeza mapato ya Serikali yatokanayo na Usajili wa Leseni za Walimu.

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa upande wa **Programu Ndogo** ya **SK010602,** Kamati inashauri Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuanzisha Idara ya Ujenzi ndani ya Wizara itakayosimamiwa chini ya Idara ya Mipango, Sera na Tafiti za Wizara ili kuweza kusimamia vyema na kufuatilia kwa karibu ujenzi wa miradi mbali mbali inayotekelezwa kupitia Wizara hii na Serikali.

**Mheshimiwa Spika,**
Kwani Kamati katika ziara zake za ufuatiliaji wa utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi wa Skuli kupitia Fedha za Ahueni ya UVIKO 19 imebaini kuwepo mapungufu mbali mbali yatokanayo na ukosefu wa wataalamu pamoja na ufuatiliaji mdogo wa Wizara, hali iliyopelekea kuwepo kwa ongezeko kubwa la fedha kwa miradi hiyo, ambapo Kamati hadi inawasilisha Hotuba hii kuna ongezeko la **Shilingi 15,000,000,000/=** (**Bilioni Kumi na Tano**) zitokanazo na kazi za ziada "*Variation of Works*".

**Mheshimiwa Spika,**
Mwisho kabisa napenda kuchukua fursa hii kukushukuru kwa mara nyengine tena kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Maoni ya Kamati yangu kwa niaba ya Kamati, pamoja na kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza.

**Mheshimiwa Spika,**
Sasa niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu waijadili na hatimae waiunge mkono bajeti hii, ili wamuwezeshe Mheshimiwa Waziri kufanikisha na kutekeleza yale waliyojipangia kwa mwaka huu wa fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika,**
Mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kuwasilisha.

............................
**(Mhe. Zawadi Amour Nassor)**
Kny. Mwenyekiti,
Kamati ya Ustawi wa Jamii,

Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar.**